Nilipozitafakari Njia Zangu

Asanteni sana, ndugu zangu, na hakika ni vizuri kuwa hapa. Asanteni. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni sana. Ninathamini hilo, inanifanya tu nijisikie vizuri unapojisikia kukaribishwa. Hakuna kitu kitamu zaidi kuliko ku—kuja mahali ambapo unajisikia umekaribishwa na uko tu nyumbani. Nami nilikuwa nikiwazia, wakati tu nilipokuwa nimesimama pale juu ya wema wa—wa watu, wema wa Mungu na watu.

2 Muda mfupi tu uliopita nilisikia ujumbe huo ukitolewa kisha Roho Mtakatifu akiujibu huo, kusikiliza Ujumbe. Halafu basi mimi . . . kisha kuwasikia ndugu hawa wakisimama na kusema mambo hayo, inanifanya tu nijisikie vizuri.

3 Halafu ilitokea leo kwamba nilichukua baadhi ya hayo matangazo. Kama Ndugu Joseph alivyowaambia jana usiku, kwa namna fulani ndio kwanza niingie tu upesi wakati huu. Nilipangiwa kwenda ng'ambo wakati uu huu, bali nilinyimwa kwa sababu ya uchunguzi fulani wa mamlaka ya kodi ninaopitia wakati huu kanisani mwangu. Na wakfu wa kanisa, jinsi inavyotubidi kuwa na namba za serikali, na kadhalika, ambalo hatukujua, kwa sababu hii maskani ni maskani isiyo na mipaka ya kimadhehebu. Hatukujua ilikubidi kupitia pilikapilika hizo, tulifikiri kwamba mlikuwa tu kanisa na mlikuwa na mashemasi, na wachungaji, na kadhalika, lakini serikali hubadilisha, walibadilisha katika mwaka wa '49, nafikiri ndivyo. Vema, nilikuwa huko nje hudumani nikihubiri wakati huo, sikujua mabadiliko yao na kile Bunge lilichofanya.

4 Kama nilivyosema jana usiku, tunazungumza juu ya Sputniki na miezi, lakini hata hatuwezi kushughulikia yale tuliyo nayo huku chini, sembuse kwenda mahali pengine, ama siwezi, kwa vyovyote vile. Kwa mtazamo wa mambo, hatufanyi kazi nzuri sana kwake, bali, kama taifa, ama watu.

5 Lakini basi, jambo lingine kuu lilikuja, kama nilivyoona hilo kwenye tangazo, nilimwambia Joseph muda mfupi tu uliopita, "Ndugu Joseph, nilifanya kosa baya sana jana jioni." Sipendi kufanya mkutano bila ya kuwa na ibada ya uponyaji angalau wakati mmoja kwenye mkutano, nami . . . tuliuweka Ijumaa usiku. Ndipo basi nikachukua hili tangazo, naye Ndugu Grant, ndugu na rafiki yangu mpendwa na wa thamani, alikuwa awe na ibada usiku huo ya kumtafuta Roho Mtakatifu, na jamani, ni—nisingetaka kuuondoa kwenye huo. Naye Joseph akasema ya kwamba Ndugu Grant alikuwa amependekeza hilo,

na wakaingia moja kwa moja kwa utamu kuutoa uwe usiku wa kuwaombea wagonjwa.

6 Sijui kama Ndugu Grant hata yupo hapa, sijamwona bado, lakini Bwana Mungu ambariki ndugu yetu kwa ajili ya nafsi yake shujaa na jinsi alivyoutoa wakati huo kwa neema.

7 Nilimwambia tungeweza kuubadilisha na kuufanya Alhamisi usiku kama tu Ijumaa, na kuachilia uendelee moja kwa moja kwa sababu nafikiri ni muhimu zaidi kwamba nafsi iokolewe, kuliko uponyaji wote ambao ungefanywa. Hiyo ni kweli. Nafsi ndiyo—ndiyo kitu muhimu, kwa sababu unaweza kuponywa magonjwa yako, hiyo ni kweli, na mateso yako yaponywe, ninajua hilo, lakini hiyo nafsi inapoponywa, ni ya Milele, lakini wakati uponyaji huu wa mwili, unaweza kuwa mgonjwa tena, bali nafsi ndiyo kitu muhimu.

8 Kwa kuwa je, uliwahi kujaribu kukadiria kwamba Uzima wa Milele ni nini? Unge—ungetoa nini kwa ajili Yake? Kama ningeweza kurudishwa kuwa mvulana wa miaka kumi na tisa, ishirini, na ningemiliki ulimwengu mzima, na kuishi miaka mia tano bila ugonjwa wala uzee, mimi . . . ama niishi mwingine, ama miaka kumi zaidi, na kuwa na shida za kila namna, na kuomba nipate chakula, na kuteswa, na kuuawa kwa sababu ya imani mwishoni bali niwe na Uzima wa Milele, ningechagua huo. Wakati miaka mia tano ilipokwisha, yote yangekuwa yamekwisha, bali Uzima wa Milele hautaisha, nitaishi Uweponi mwa Kristo milele. Kamwe hatujui kile kilichofunikwa katika hazina hiyo ambayo Mungu ametupa.

9 Ndugu Rasmussen, hakika ni vizuri kukuona tena usiku wa leo. Tumekuwa na ushirika mwingi pamoja, na wahudumu mbalimbali. Basi nafikiri tutakuwa na kiamshakinywa hivi karibuni sana, na—nasi tutaninii, huenda tukaweza kupeana mikono, na—na kuwa na wakati wa ushirika na kundi hili lote zuri la watu ambao daima wanashawishi na kuomba kila mwaka nije kwenye ushirika wao, inanifanya nijisikie vizuri sana.

10 Mke wangu pia alitaka kuwashukuru ninyi nyote kwa makaribisho yenu. Na jana usiku, hakuingia jana usiku. Tumepata mvulana mdogo, Joseph. Ni wangapi wanaokumbuka nikizungumza ya kwamba Joseph angekuja miaka kadhaa kabla hajafika hapa? Miaka sita, Bwana alinionyesha kuja kwake. Naye ni mvulana kabisa, yeye ni maskini mwanamke.

11 Mtu fulani, nilikuwa nikizungumza hapa wakati fulani uliopita, na, kwenye mkutano wa Kihispania, nami nikasema, “Hili ni kusanyiko la kimataifa,” nikasema, “Mimi ni Mwairishi, mke wangu ni Mjerumani, mtoto wangu mchanga ni Mhindi, nami ninawazungumzia Wahispania.”

Baadaye, msichana mdogo wa Kihispania akasema, “Ndugu Branham, hivi hufikiri kwamba mtoto wako amepauka kidogo asingekuwa Mhindi?”

Nikasema, “Ni Mhindi tu kwa matendo,” kweli mvulana kwelikweli.

12 Muda umeenda kidogo, na kwa hiyo hatutachukua muda mwingi kupita kiasi. Basi Bwana na atubariki sasa tunapoinamisha vichwa vyetu kunena Naye.

13 Baba Mwenye Neema sana, kamwe hatuwezi kupata maneno yoyote ya kuelezea hisia zetu moyoni mwetu. Kama ilivyosemwa na mtu mmoja siku moja mkutanoni, kwamba angeweza kunena katika lugha saba mbalimbali, na angeweza kunena kwa ufasaha, lakini alipofika karibu na Wewe usiku mmoja, asingeweza kupata maneno yoyote ya kuelezea jinsi alivyojisikia, kwa hiyo Wewe ukampa lugha mpya kuonyesha hisia zake Kwako. Hivyo ndivyo tunavyojisikia, Bwana, hakuna maneno ambayo tungeweza kuunda katika mawazo yetu kusema jinsi tunavyokupenda Wewe, na kukushukuru Wewe kwa ajili ya kile umekuwa kwetu. Wala tusingeweza kuwa na kicho cha kutosha, wala hata tusingeweza kuwazia mawazo mazito ya kutosha kuja Kwako kukuomba uendelee kuwa pamoja nasi. Loo, tunakuhitaji, Bwana. Kama vile mtunzi wa nyimbo alivyosema:

> Ninakuhitaji Wewe, loo, ninakuhitaji Wewe,
> Kila saa ninakuhitaji Wewe.

14 Hivyo ndivyo tunavyojisikia, Bwana, kwa hiyo tukaribie sasa tunapoketi baada ya siku kuu ya—ya kunena na madhihirisho ya baraka Zako. Nasi tumekuja usiku wa leo kusikiliza Neno tena. Tungeomba ya kwamba ungeyachukua maneno ya mtumishi Wako na kuyanenea mioyo ya watu Wako. Ndipo tutakapoondoka usiku wa leo, mioyo yetu na ijazwe sana na upendo Wako mpaka tutaondoka hapa tukiwa na azimio la kukutumikia Wewe zaidi ya wakati wowote maishani.

15 Na kama kungekuwako na mgeni, ambaye amekuja miongoni mwetu usiku wa leo, asiyekujua katika ubatizo wa Roho Yako, wala hajakujua Wewe kwa maungamo ya imani, jalia hii iwe ndiyo saa ambayo wataisema hiyo *ndiyo* moja ya Milele kwa Mungu na kutoa yote waliyo nayo. Na kama hilo limefanywa wala bado hawajampokea Roho Mtakatifu tangu walipoamini, jalia huu uwe ndio usiku ambao watapokea Karama ya Mungu maishani mwao.

16 Kama kuna wagonjwa miongoni mwetu, Bwana, jalia watoke hapa usiku wa leo wakishangilia na kumshukuru Mungu kwa imani mpya waliyoipata na afya. Tunakutegemea Wewe, Bwana, kwa kuwa Wewe umeahidi ya kwamba utatujaza na mambo mema. “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa.” Sasa nena na mioyo yetu kulingana na mahitaji yetu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

17 Nimechagua somo usiku wa leo: *Nilipozitafakari Njia Zangu*. Ningetaka kusoma baadhi ya Maandiko, ama, kifungu cha Maandiko kinachopatikana: Zaburi ya 119, na kifungu cha 59:

Nalizitafakari Njia Zangu, na miguu yangu nalizielekezea shuhuda zako.

18 Daudi alikuwa katika shida wakati alipoandika Zaburi hii. Tunaambiwa kwamba ilikuwa ni wakati ambapo Sauli alikuwa akitishia kumwua, nayo nyumba yake ilikuwa ikichunguzwa, Watu wa Sauli walikuwa wamevizia, wakiangalia wamwone Daudi akitoka nje, ndipo wangemwua.

19 Nami ninaweza tu kuwazia usiku wa leo, nikimwona Daudi akitembea huku na huku, huku na huku sakafuni akiiminya mikono yake. Kwa kawaida wakati mtu anapopata shida ndipo atakapomgeukia Mungu. Ni vibaya sana kwamba inabidi yahitajike mambo hayo kumfanya mtu atambue kwamba yeye ni mwenye dhambi, au yuko mbali na Uwepo na baraka za Mungu, bali Mungu hulifanya hivyo.

20 Nami ninaweza kumwona wakati akitafakari, na kwa ghafula, wema wa Mungu unatokea, naye anaanza kuimba kwa sauti:

Nilipozitafakari njia zangu, na kuzielekezea miguu yangu shuhuda zako.

21 Miezi michache iliyopita katika mji wetu mdogo wa Jeffersonville, Indiana, nilipigiwa simu na mama mmoja nishuke nikazungumze na hakimu wa ma—mahakama, ambaye ni rafiki yangu wa karibu, na kumtetea mwanawe, kwani alikuwa anaenda kufungwa gerezani kwa kuiba gari. Ndipo nikampigia huyo hakimu simu, na nikasema, "Naomba kuzungumza nawe asubuhi, faraghani, muda kidogo tu kabla ya ile kesi."

Naye akasema, "Hakika."

22 Basi nikaenda ofisini mwake na kubisha mlango, nao wakafungua mlango, akamwomba huyo mtu atoke nje, naye akanisalimia vizuri sana kwa mkono, na kusema, "Una nini akilini mwako asubuhi ya leo, Ndugu Branham?"

23 Ndipo nikasema, "Hakimu, ninge—ningetaka kukuuliza jambo fulani, huku ukijua ya kwamba wewe mwenyewe utasimama siku moja mbele ya Hakimu mwenye haki, nami najua ya kwamba inakubidi kuwa mwaminifu katika maamuzi yako, kadiri ujuavyo, lakini yule mvulana utakayeendesha kesi yake katika dakika chache zijazo, mamaye alinipigia simu jana usiku na kusema ya kwamba mwanawe alilia begani mwake sana, na kusema, 'Mama, ikiwa Mungu atanijalia tu kuachiliwa, nitamtumikia siku zote za maisha yangu.'"

24 Hakimu akaniangalia, akasema, "Billy, unajua nini? Kamwe sijampeleka mtu gerezani bado, pasipo yeye kutaka kuwa mhubiri kabla hajaondoka."

25 Mnaona, ni wakati tunapokuwa katika shida, ndipo tunaanza kuwazia juu ya Mungu. Ni vibaya sana kwamba hatuna budi kuwa hivyo, lakini ndivyo ilivyo.

26 Wakati Israeli walipopata shida walipokuwa wamemwacha Mungu, na kuziendea sanamu, na kufanya mambo ambayo hawakupaswa kufanya, ndipo walipomgeukia Mungu na kulia, walitoa dhabihu za kondoo na—na wanyama, na—na kulia mchana na usiku wapate rehema. Halafu basi jambo la kushangaza walilokuwa nalo Israeli, ndivyo lilivyo na kanisa siku hizi, Mungu atawaokoa, halafu baada ya yote kwisha, wanasahau yote kulihusu.

27 Kama Mungu alikuwa na rehema sana kumsamehe mtu dhambi zake, na kumpa Uzima wa Milele, anapaswa kuwa na kicho sana mbele za Mungu siku zote za maisha yake hata kamwe hataielekeza miguu yake mbali na shuhuda za Mungu, anapaswa kutembea kwa unyofu siku zote mbele za Mungu. Lakini mambo ni hivyo tu, wanafanya hivyo.

28 Inatupasa sisi sote, wakati hatuna shida, kumtafuta Mungu. Si vema kungojea mpaka tutakapoingia hatarini ndipo basi tumtafute Mungu, ni vema kumtafuta sasa, kwa maana imeandikwa ya kwamba Yeye ni Msaada unaoonekana tele wakati wa shida.

29 Ninaweza kukumbuka hadithi fulani, na mke wangu huko nyuma anaikumbuka zaidi kuliko ninavyoikumbuka, nadhani: Kwenye fungate yetu, ilinibidi kutumia wakati mdogo maradufu. Tulipokuwa kwenye fungate yetu, hatukuwa ila na pesa kidogo tu, kwa hiyo ni—nilimpeleka huko New York kuona Maporomoko ya Niagara, na wakati tukiwa huko juu nikaenda kuwinda.

30 Nami nikamwacha katika kibanda kidogo asubuhi moja, nami nilifikiri nilikuwa Mhindi mzuri sana nisingeweza kupotea mwituni, basi nikatangatanga, nikimwambia ningerudi wakati fulani, naye ni msichana wa mjini, hakuwa amewahi kuwa milimani maishani mwake. Nami nikasema, "Wewe choma viazi kidogo juu ya moto, nasi tutakula chom-. . . viazi vilivyochomwa, na chumvi, pilipili, ukazitie, na kipande kidogo cha siagi." Nikasema, "Tutakuwa tu na yubile halisi. Nitarudi saa nane."

31 Nami nikaweka mkono wangu juu ya kichwa cha Billy, ambaye alikuwa ni mtoto mdogo tu wakati huo mwenye umri wa miaka mitano hivi, halafu nikashuka kupitia mwituni. Nilipokuwa nikitangatanga kwenye ule msitu mkubwa mno, nilikuwa nikifuata mburuzo wa dubu. Baada ya kitambo kidogo nikaona kitu upande wa pili wa safu ya vilima, nami nikavuka safu nyingine ya vilima, na safu nyingine ya vilima, nikashuka chini, ambayo inaitwa Majitu, iko kwenye Adirondacks. Ndipo nikampiga risasi kulungu, kulungu mkubwa, mkubwa mno,

nami nikasema, “Huyo ni bora kuliko dubu. Sasa nitarudi nyumbani.” Ndipo nikaona, mawingu ya dhoruba yametanda chini, ndipo nikasema, “Sasa, nilishuka chini moja kwa moja *hivi*.”

32 Sasa, mtu yeyote ambaye amewahi kuwa mwituni anajua, ni wakati wa kuketi chini wakati mawingu ya dhoruba yanapokuja, maana kuna ukungu, hujui unakoelekea.

33 Lakini nilipofika juu zaidi, nikifikiri nilikuwa nikienda sawa, nilijikuta nikitembea mbali sana nikijaribu kutafuta mahali pa kutokea, nikarudi mahali nilipompiga risasi yule kulungu, nilifanya hivyo mara tatu mfululizo. Sasa, Wahindi wanaita hayo “matembezi ya mauti.” Unatembea kimzunguko, unafikiri unaendea njia moja lakini unarudi mahali pale pale.

34 Dhoruba ilikuwa tayari inapiga, theluji ilikuwa inaanguka, nami nikawazia, “Nifanye nini sasa? Nina mke na mtoto mchanga katika msitu huu, kamwe hawajawahi kuwa mwituni maishani mwao, nao wata—watakufa usiku wa leo.”

35 Kwa kawaida, ningetafuta pango, na kuingia ndani yake, na kungoja mpaka dhoruba ilipokwisha, siku moja ama mbili, nitoke, na kuona mahali nilipokuwa, na kuendelea mbele. Lakini wao hawakujua jinsi ya kujishughulikia wenyewe.

36 Ndipo nikasema, “Sasa, ngoja kidogo, unarukwa na akili tu.” basi unapofanya hivyo, unashikwa na homa na basi umepotea, ndipo hutawahi kamwe kupata njia ya kutokea, unajitumbukiza mautini, sana sana.

37 Vema, nilijua nilikuwa nikitembea kimzunguko, lakini ilikuwa ni mzunguko gani? Upepo ulikuwa ukija usoni mwangu wakati nilipoenda kumpiga risasi yule kulungu, halafu basi nilipokuwa nikirudi upepo ulikuwa usoni pangu tena, kwa hiyo nisingeweza kujua mwelekeo wa jumla kwa sababu ulikuwa ukizunguka-zunguka kwenye vilele vya miti.

38 Basi nikasema, “Vema, ninaenda njia moja iliyonyooka tena.” Kisha nikasema, “Sitageuka, nitaenda moja kwa moja, nami ninajua ya kwamba niko sahihi. Mimi ni mtu hodari sana wa mwituni nisingeweza kupotea mwituni.” Basi nikaanza, kwa namna fulani nikijipa moyo, hicho ni kiakili, “Siwezi kupotea, kwa sababu mimi ni mwindaji hodari sana.” Basi nikaanza kwenda, ndipo nikaanza kutambua ya kwamba nilikuwa nimepotea.

39 Hivyo ndivyo tunavyokuwa wakati mwingine tunapofikiri tunajiunga na kanisa tuko sawa, lakini kuna kitu kinachotwambia tumepotea. Ngoja mpaka mauti yatakapokupiga, ndipo uone kile unachowazia, afadhali uwe na hakika sasa.

40 Basi nilipoanza kwenda, kwa uaminifu moyoni mwangu, ningeweza kusikia Sauti ikinena nami, ikisema, “Bwana ni Msaada utakaoonekana tele wakati wa shida.”

41 Ndipo nikawaza, “Sasa ninarukwa na akili.” Ndipo nikatambua kwamba nilikuwa nimepotea kabisa. Basi nikapiga magoti na, juu ya kofia yangu, na kuiegemeza bunduki yangu kwenye mti, na kusema, “Bwana Mungu, nimepotea na ninakuhitaji Wewe.”

42 Ndipo nilipoinuka, nikasema, “Sasa nitaenda mbele moja kwa moja tena.”

43 Basi nilipopiga hatua mbili ama tatu mkono ukawekwa begani mwangu, nami nikageuka kuona ilikuwa ni nini papo hapo kwenye wakati mzuri wa kuona mawingu yakirudi nyuma na kuona ule mnara ulio juu ya Mlima Hurricane. Nilikuwa nikienda moja kwa moja Canada, ndipo Bwana akanirudisha kwenye ule mnara. Nilisimama nimeelekea kabisa kwenye mnara ule, nikalia, na nikapaza sauti sifa za Mungu, kwa kuwa nilijua alikuwa ameielekeza miguu yangu njia sahihi tena.

44 Hiyo ilikuwa dakika kuu kwangu, lakini haikuwa nusu dakika siku moja wakati alipouelekeza uso wangu Kalvari nilipokuwa nimepotea, kamwe siwezi kuisahau dakika hiyo. Hebu tuje wakati tukiwa na akili timamu.

45 Wakati fulani uliopita mvulana mdogo mweusi aliingia mbio mkutanoni wakati wito wa madhabahuni ulipokuwa unatolewa, alikuja kutoka nje, ndipo akapanda juu, naye akasema, “*Mimi* taka kuwa Mkristo usiku wa leo.”

“Mbona, bila shaka, daima tunafurahi kuona jambo hilo.”

46 Kisha kasema, “Sababu ya mimi kutaka kuwa Mkristo, nimekuwa mzururaji.” Kisha kasema, “Nilikuwa huko nje nikiranda-randa wakati mmoja, na, huko Northwoods,” kisha kasema, “Nikaishiwa na pesa.” Tena kasema, “Nilijiajirisha kwenye kambi ya ukataji miti ambako kulikuwa na mwanamke mkongwe, mweusi aliyefanya upishi, nami nilikuwa nimsaidie na—na halafu kumwoshea vyombo, na kadhalika, nipate pesa za kutosha kuendelea mbele.”

47 Kasema, “Tulilala kwenye chumba kidogo cha nyuma chenye kipande kikubwa cha turubai kutenganisha sehemu yake na sehemu yangu.” Kisha kasema, “Usiku mmoja huku nimejifunika kichwa, niliamshwa na sauti zilizokuwa zikinena kwa sauti kubwa karibu na dirisha langu. Ndipo nikakifunua kichwa changu,” kisha akasema, “Nilimsikia mtu mmoja akisema, ‘Jim, hebu tuharakishe kurudi kibandani upesi tuwezavyo, kwa sababu tunaweza kufagiliwa tuingizwe katika Umilele katika dakika chache zijazo, kwa kuwa kimbunga hicho kinaelekea moja kwa moja huku.’”

48 Kasema, “Wala nisingefanya chochote ila kustaajabu niliporuka dirishani na kutazama na kuona wingu hilo refu lenye umbo la dohani, na mfululizo mmoja tu wa ngurumo na radi. Na kuona wakati radi, miti iking’olewa kutoka mizizini, na huo mkia mkubwa, mrefu wa nyoka ulikuwa ukija moja kwa moja kuelekea kibanda chetu.”

49 Kasema, “Nilisikia turubai ikipasuka, ndipo maskini yule mwanamke mkongwe, akasema, ‘Mwanangu, njoo kwangu, nina taa iliyowashwa hapa.’” Kisha kasema, “Nilienda mle, naye akasema, ‘Je, wewe ni Mkristo?’”

Kasema, “Nilisema, ‘La, mimi si Mkristo.’

“Kasema, ‘Uliwahi kuomba?’

“Kasema, ‘La, sijawahi kuomba.’

“Kasema, ‘Vema, afadhali uombe, kwa maana hivi vimbunga huangusha kila kitu chini ardhini.’”

50 Kasema, “Kasisi, nilipiga magoti karibu na mwanamke huyo mkongwe kwenye kile kijisanduku ambapo ile taa iliwekwa, ila niliogopa sana nisingeweza kuomba.” Akasema, “Nisingeweza kuweka mawazo yangu sawa.” Naye akasema, “Kila wakati ningeanza kuomba, mti ungeng’oka na kukigonga kibanda, madirisha yangetoka.” Akasema, “Niliogopa sana nisingeweza kuomba.” Akasema, “Sasa, jambo lote nililoweza kufanya lilikuwa ni kuketi na kumwangalia yule mtakatifu mzee mtulivu asiyekuwa na wasiwasi hata kidogo kuhusu chochote ulimwenguni, daima akizungumza na Mtu fulani ambaye alikuwa anamfahamu. Nami nikasema, ‘Bwana, ninahofu sana siwezi kuomba, lakini kama utanijalia tu kuishi, nitaomba baada ya jambo hili.”

51 Mnaona, inahitaji matatizo wakati mwingine kutufanya tutambue, kuielekeza miguu yetu kwa Mungu, kujikabidhi Kwake.

52 Ninaamini ilikuwa ni Ayubu aliyezitafakari njia zake, naye alitaka kuhakikisha, si njia zake tu, bali njia za watoto wake. Naye akapitia njia pekee ya Mungu ambayo Mungu aliwahi kumwandalia mwanadamu: sadaka ya kuteketezwa na chini ya damu. Wengi wenu mna hakika ya kwamba . . . Mmesoma hadithi ya Ayubu, naye alisema, “Watoto wangu wamekuwa wakifanya karamu, na labda wametenda dhambi, nitatoa sadaka kwa ajili yao.” Alitaka kuwa na hakika wakati alipokuwa kawaida na sahihi.

53 Mnajua nafikiri kama mama na baba usiku wa leo katika hii nchi yetu nzuri, kama wangetumia muda mwingi zaidi magotini mwao wakiomba, wakiwaleta watoto wao kwa Mungu kwa njia ya maombi, badala ya kuwa huko nje kwenye karamu hizi wakinywa pombe na kuzurura, tungekuwa na uhalifu kidogo wa vijana.

54 Naye Ayubu alipitia njia ya damu, kumwagwa kwa damu. Huo ndio msingi pekee ambao Mungu aliwahi kushirikiana na mwanadamu, ni juu ya msingi wa damu iliyomwagika; hakuna njia nyingine ambayo Mungu atashirikiana na watu, ila tu kwa damu iliyomwagika. Katika Agano la Kale, ilibidi Israeli waje mahali pamoja pa kuabudia, hapo palikuwa chini ya damu iliyomwagika.

55 Ndipo wakati shida ilipompata Ayubu, angeweza kupiga mayowe, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Naye angeweza kupiga mayowe, "Ajaponiua, hata hivyo nitamtumainia." Kwa nini? Alijua njia ya kuendea alipopata shida.

56 Baadhi yetu hupitia njia zingine. Katika wakati huu wa fadhaa tunaoishi watu wengi sana wanawaendea wataalamu wa magonjwa ya akili, mpaka Wakristo wanamwendea mtaalamu wa magonjwa ya akili; naye mtaalamu wa magonjwa ya akili hana budi kumwendea mtaalamu wa magonjwa ya akili. Tuzielekeze njia zetu kwa Mungu, Yeye ndiye Mponya wetu. Kama mioyo yetu haituhukumu, basi tuna hakikisho hili: Mungu hujibu maombi.

57 Ayubu angeweza kusema kwa moyo wa kweli, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai." Naye akazitafakari njia zake, akamgeukia Yeye.

58 Daudi, baada ya kufanya makosa na kumchukua mke wa Uria Mhiti, Bath-sheba mrembo sana, naye alikuwa anaenda kuwa baba wa mtoto wake, naye alikuwa amemsababisha mumewe shujaa kuuawa vitani, lakini wakati nabii, Nathani, alipoingia na kumfunulia dhambi zake, ndipo Daudi alipozitafakari njia zake, naye akageuka akatubu amevaa nguo za magunia na majivu. Hiyo ndiyo njia ya kugeuka. Mungu alimsikia. Mungu daima atamsikia mwanamume ama mwanamke ambao wataelekeza miguu yao kwenye shuhuda Zake.

59 Daudi alistahili kufa, naye alikuwa ametangaza kifo chake mwenyewe, bali Nathani alisema, "Hakika, hutakufa." Kwa kuwa alijua Daudi alimjua Mungu, na alijua ya kwamba alikuwa amefanya kosa, alikuwa amemchafua mke wa ndugu yake.

60 Nashangaa usiku wa leo, wala nisingesema hili, lakini labda kunaweza kukawa na Daudi mwingine aliyeketi hapa usiku wa leo ambaye ana hatia kama Daudi alivyokuwa nayo. Unapozima taa yako usiku, unaona uso wa ndugu yako, mwanamume ambaye ulimchafulia mke wake mpendwa, au kuvunja nyumba yake, akipepesuka kando ya ukuta wako, ama mwanamke fulani aone nyumba ya mwanamke ambayo ameivunja kwa kutoroka

na mumewe. Inapaswa kukuleta kwenye toba umevaa nguo za magunia na maungamo!

61 Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo ni maungamo, na kurekebisha, na kurudi kwenye shuhuda za Bwana Mungu, kuna rehema na msamaha. Inaonekana kwamba ingewatesa watu, wakiendelea, wakijua ya kwamba unatembea saa baada ya saa usoni pa mauti. Kwa nini tuendelee na ubinafsi, na tamaa, na uovu, na—na macho yetu kwenye mambo ya ulimwengu? Wakati umewadia wa kuzirudia shuhuda za Mungu. "Nilizitafakari njia zangu, miguu yangu nikaielekeza kwenye shuhuda Zako."

62 Ilikuwa ni nabii Yakobo aliyekuwa amefanya makosa, tena alikuwa amemdanganya baba yake kipofu kwa sababu ya haki ya mzaliwa wa kwanza, siku moja moyo wake ulianza kutamani kurudi kwenye nchi ya uenyeji wake. Naye hapana shaka alifikiri wakati huo wote yalikuwa yamefunikwa, lakini alipoanza kukaribia nyumbani, alisikia ya kwamba Esau alikuwa anakuja kukutana naye, ndipo akazitafakari njia zake za udanganyifu, naye akaomba usiku kucha ng'ambo ya mto. Alipotafakari jinsi alivyomdanganya ndugu yake, ilimwalika kwenye maombi ya usiku kucha. Mungu anajua hayo ndiyo kanisa linahitaji.

63 Nakumbuka wakati kanisa lilikuwa likitoa wito wa mikutano ya maombi ya usiku kucha, ndipo wakati mahubiri yalipotolewa, hapakuwapo na jicho kavu kanisani, kila mtu alilia na kupaza sauti mbele za Mungu. Na leo hii linaonekana kana kwamba ni legevu sana, hata watu wanaendelea tu kuishi vyovyote watakavyo, na bado wanasema wao ni Wakristo. Nashangaa kama hatukaribii Nyumbani, afadhali tuzitafakari njia zetu, na kuielekeza miguuu yetu kwenye shuhuda Zake.

64 Ilikuwa ni Musa, yule nabii mwenye nguvu, aliyekuwa amegeuka kuwa mchunga kondoo mzee, aliyekuwa akitangatanga nyuma ya mlima siku moja kwenye ujia mdogo wa kale ambao kondoo walikuwa wametengeneza, labda aliufahamu sana, lakini asubuhi hiyo ilikuwa tu tofauti kidogo na asubuhi zingine, kulionekana kuwa na Kitu fulani kilichomzunguka.

Mnajua, Yesu alisema wakati mmoja, "Wakinyamaza, miamba itapiga kelele." Nashangaa kama Malaika hawakuwa wakimhubiria.

65 Kwa ghafula, akaanza kuzitafakari njia zake, jinsi ambavyo alikuwa ameshindwa maishani, na alikuwa amejaribu kupata usalama wakati watu wake walipokuwa utumwani.

66 Mungu, jalia kwamba moyo wa kila mhubiri hapa ndani utapata mzigo huo. Tunawezaje kupumzika Sayuni wakati ulimwengu umefunikwa na dhambi na washiriki wa kanisa wakiishi katika dhambi? Tunawezaje kutulia wakati kanisa limevunjwa-vunjwa na kanuni za imani na madhehebu, na

udugu umetenganishwa, nao watu wanakuwa wa kilimwengu, wakati Mungu anapohitaji utakatifu, la sivyo hakuna mtu atakayemwona Bwana?

67 Musa akaanza kuzitafakari njia zake, jinsi ambavyo alikuwa ameenda kombo katika elimu yake mwenyewe na mafunzo, naye alijua kulikuwa na wito wa Mungu juu ya maisha yake, bali alikuwa amejaribu kuutekeleza kwa njia yake mwenyewe.

68 Wengi wetu wahubiri tunaingia katika tatizo hilo, wito wa Mungu maishani mwetu, kisha tuondoke tukapate elimu inayotwambia ya kwamba siku za miujiza zimepita, wala hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, ati huo ulikuwa ni wa siku zilizopita. Mungu akujalie uzitafakari njia zako! Mungu yuyo huyo aliyeandika Neno hilo angali hai na anakuwajibisha Kwake. Ni kosa!

69 Mungu hana kikomo, na wakati anaponena, halina budi kuwa kamilifu, Yeye hawezi kubadilika. Hatuwezi kulibadilisha Neno la Mungu, inatubidi kubadilisha mawazo yetu kwa mawazo Yake. Hebu nia ya Kristo iwe ndani yako, ndipo utawazia kama Yeye anavyowazia.

70 Na wakati akianza kuwazia juu ya mambo hayo, ninaweza kumwona amechanganyikiwa kabisa. Hakuna mtu anayeweza kuja mbele ya maisha yake ya zamani, ila anayevurugika juu yake. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atamleta kila mwanadamu humu ndani sasa kurudi kwenye mambo yako yaliyopita na kuyaangalia, kisha ugeukie shuhuda Zake.

71 Ndipo alipoanza kutafakari, ninaweza kumwona yule mzee mwenye ndevu nyeupe zinazoning'inia, lakini akasema, "Nimeyaharibu maisha yangu, nina umri wa miaka themanini, na laiti ningeyatafakari nilipokuwa kijana na ningefanya jambo sahihi! Lakini sasa ni mbali sana." Na machozi makubwa maangavu yakitiririka kwenye masharubu yake meupe.

72 Na yapata wakati huo, alipokuwa akizitafakari njia zake, kulikuwa na kelele za kishindo kando ya kilima. Basi alipokuwa akizitafakari njia zake, alisema, "Nitageuka nione jambo hili alilofanya Mungu." Ninatumaini ya kwamba Mungu atakileta kichaka hicho kinachowaka moto katika umbali wa kusikia wa kila mtu hapa usiku wa leo, tunaweza kuzitafakari njia zetu.

73 Basi ilimbadilisha Musa wakati alipoigeuza miguu yake kutoka kwenye njia ya kondoo na wanyama wa mwituni kuelekea njia ambayo Mungu alikuwa amemwongoza kupitia Bahari ya Shamu na kwenda kwenye nchi ya ahadi. "Kuzitafakari njia Zake," inatufaa kuzitafakari njia Zake.

74 Baada ya jogoo kuwika mara tatu na Petro kuutazama uso wa Bwana Yesu, alianza kuzitafakari njia zake, na yale aliyokuwa amemfanyia Bwana wetu. Ndipo unabii na Neno la Bwana likaonekana waziwazi kwake, kwa kuwa alijua Mungu alikuwa amesema. Mungu yeye yule aliyemwambia hivyo,

ametwambia la kufanya. Ilifanya nini wakati alipoyatafakari yale aliyokuwa amemtendea Yesu, na jinsi alivyokuwa amemkana mbele ya watu mashuhuri, na jinsi ambavyo alikuwa amejaribu kuwa mmoja wa hao walimwengu, na kujaribu kutenda kama hao wengine? Alipozitafakari njia zake, ilimpeleka gizani akalie kwa uchungu.

75 Ninaamini ni wakati wa kuwika kwa jogoo sasa kusudi kanisa la Mungu aliye hai lipate kuwa peke yake pamoja na Mungu na kulia kwa uchungu wa machozi, na kusema, "Mungu, unirehemu." Hapana shaka kuna wanaume na wanawake hapa usiku wa leo, wavulana na wasichana wanaohitaji kitu kile kile, sisi sote tunakihitaji, peke yetu na Mungu. Tuzitafakari njia zetu tunapoenda, tuielekeze miguu yetu kwenye shuhuda Zake.

76 Naam, Yuda ndiye aliyekuwa amesimama karibu na kuhani mkuu kupokea fedha kwa ajili ya kumsaliti Bwana Yesu. Bila shaka ningechukia kupachukua mahali pake. Lakini kuna watu huku Chicago usiku wa leo walio na hatia zaidi kuliko Yuda Iskariote. Alikuwa akipokea hongo; watu wengi wamepata mshahara, na gari la Kadilaki, na nyumba kubwa kubwa, wakiziuza kanuni za Mungu. Wanauonea aibu ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanauonea aibu utendaji wa Roho Mtakatifu wa Mungu, wao ni watu mashuhuri sana, hilo linawafanya wajiunge na kanisa, wanafanya hivyo kwa sababu wanaogopa kuzaliwa upya.

77 Ninasema hili katika umati uliochanganyikana, bali nataka mnielewe kama ndugu yenu: Mtoto mchanga anapozaliwa, kama ni sakafuni, kama ni kwenye mto wa majani makavu, ama kama ni juu ya, katika chumba cha hospitali kilichopambwa, ni mchafuko vyovyote unavyolichukua, bali linaleta uhai. Hivyo ndivyo kuzaliwa upya kulivyo, ni mchafuko, bali huleta Uzima, huleta Uzima wa Milele. Amina. Huleta Uzima, nao Uzima, sijali uko kwenye kiwango gani, ninataka kuwa na Uhai huo, ambapo tunaishi milele. Watu hujiunga na makanisa kukwepa jambo hilo, wanauza haki zao za mzaliwa wa kwanza kama Yuda alivyofanya.

78 Ndipo akasikia kuchezacheza kwa fedha hiyo ikichezacheza mikononi mwake, ndipo akalia, "Nimeisaliti Damu isiyo na hatia." Sitaki kitu chochote kisimame kati yangu na Bwana namna hiyo mwishoni mwa safari, natumaini hakitasimama, ninyi. "Nimeisaliti Damu isiyo na hatia." Naye akashika njia ya mkato, akachukua kamba akaenda, akajinyonga.

79 Unapoyatafakari mambo yako yaliyopita, ama yatakusukuma kwa Mungu au yatakupeleka mbali na Mungu. Huenda ukachukua njia ya dhambi, kurudi nyuma, kuvuta sigara, kujaribu kuipulizia mbali, huenda ukaelekea kwenye baa, na kununua wiski na kujaribu kuisahau kwa kunywa wiski, wakati umejitia najisi, na kuwatia wengine najisi, na

kusema uongo, na kuiba, na kudanganya, ama kuikana Injili unayojaribu kuiwakilisha, kuwa na mavazi ya kupendeza na kuonekana kama hao wengine, na kutenda kama watu wa siku hizi. Mungu anakutaka uwe tofauti, Yeye anahitaji tofauti. Utakuwa na hatia tu kama vipande thelathini vya fedha.

80 Unaweza kupitia njia ya mkato, hakika, lakini hapajakuwapo na moja. Angalia nyuma katika nyakati za Biblia, wale waliomjia walipozitafakari njia zao kama Petro, alipata rehema; wale waliopitia njia ya mkato wako katika Umilele, huko nje mahali fulani bila Mungu, bila tumaini, bila Kristo. Shika njia ya kwenda Kwake, iko wazi. Hiyo ni kweli.

81 Yule askari wa Kirumi, baada ya kumchoma ubavuni kwa mkuki wake na kuona maji na Damu ikibubujika, na kuona jua likitua katikati ya mchana, miamba na milima ikipasuka, na kusikia ngurumo, na kuona radi bila wingu, alijipigapiga kifuani, na kusema, "Hakika huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu!" Alitafakari njia zake, akaona yale aliyokuwa amefanya, na huyo akashuka chini ya msalaba, ndivyo tunavyoambiwa, alizitafakari njia zake, kisha akazigeukia shuhuda za Mungu.

82 Pilato, baada ya kujaribu kuiosha mikono yake ajiondolee lawama ya Yesu, miaka kumi ilipita, naye alikuwa angali anajaribu kuiondoa Damu ya Kristo mikononi mwake; labda miaka kumi tangu usiku wa leo utakuwa ukijaribu kuuondoa Ujumbe huu mikononi mwako. Lakini alinawa, na akanawa, na akanawa, wala hapakuwa na njia ya kuiondoa, alijaa majivuno mno asingeweza kumgeukia yule Mtu aliyekuwa amemwua. Hatimaye akajitumbukiza katika kidimbwi cha maji huko Uswisi akafa, ambapo hekaya ni, kwamba katika kila Ijumaa Kuu maji ya samawati huvurugika.

83 Sijui usiku wa leo, kama unatafakari juu ya njia zako, sijui kama umekuwa ukitafakari huko nyuma moyoni mwako jambo ambalo umefanya na njia ambayo umepitia. Kama unatafakari, nawe umehukumiwa, usichukue njia ya mkato ya kwenda kujiunga na kanisa, ama uende ukafanye *hiki*, ama unywe pombe hata ufe, ama chochote kile. Vema, hebu nikwambie jambo fulani:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Yule mwizi aliyekuwa akifa (alizitafakari njia zake) na akafurahi kuona
Chemchemi hiyo katika siku zake;
Hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

Tangu kwa imani nilipoona kijito hicho
Kilichosababishwa na majeraha Yako,
Upendo wa kukomboa umekuwa ndio mada yangu,
Na utakuwa hata nitakapokufa.

Kisha katika wimbo mzuri zaidi, mtamu zaidi,
Nitaimba nguvu Zako za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kithembe, unaogugumiza
Utakapolala kimya kaburini.

84 Mkimbilie, kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako. Na tuinamishe vichwa vyetu. Tuzifafakari njia zetu.

85 Bwana, tufanye nini? Ama tuzitafakari njia zetu sasa na kuzirekebisha, au labda kabla ya asubuhi tutakuwa tumechelewa sana, mioyo yetu itakuwa inapigapiga, mauti yatakuwa yanakutana nasi, nasi tutakuwa kama yule kijana mweusi, yeye . . . tusingeweza kuomba, lakini wakati tukiwa watu wa kawaida, wakati tumeketi hapa huku wimbo wa utangulizi ukicheza, *Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu*, jalia tuzitafakari njia zetu na kuzigeukia shuhuda Zako.

86 Iongoze miguu yetu kwenye njia hiyo ya Uzima, njia ile iliyojaa Damu ambayo Yesu alikanyaga kote kutoka kwenye ukumbi wa hukumu wa Pilato hadi Kalvari. Jalia tujikane wenyewe, tuchukue msalaba Wake, na kumfuata. Na tunapotafakari, jalia Roho Mtakatifu anene na mioyo yetu, na jalia tugeuke kutoka kwenye njia zetu za kichoyo hadi njia za Bwana.

87 Na sasa, huku vichwa vimeinamishwa na kila mtu akiomba, kama unazitafakari njia zako wala hujisikii vizuri sana juu yake, hebu tuje sasa hivi, hebu na tusimame moja kwa moja kwa miguu yetu, tukisema, "Bwana, ninazitafakari njia zangu." Mungu akubariki, ewe kijana. "Ninazitafakari njia zangu, nami ninageuka sasa hivi. Loo, nimempokea Roho Mtakatifu muda mrefu uliopita, lakini kumekuwa na mambo mengi sana ambayo nimefanya, ninazitafakari njia zangu, ninajua nimekosea, na miguu yangu ninaielekeza kwenye shuhuda Zako sasa hivi ninaposimama. Ninatamani maombi ya kanisa hili mniombee sasa. Ninazigeukia shuhuda Zako, Neno Lako, Ee Bwana, na shuhuda Zako ni hizi: 'Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe.'"

88 Iko pia katika shuhuda: "Ukiificha dhambi yako, hutafanikiwa, bali kama ukikiri dhambi zako, utapata rehema." Wewe unayetaka msamaha wa yote uliyofanya, nawe unatoa ahadi yako ya maisha yaliyowekwa wakfu kwa Mungu tangu usiku wa leo na kuendelea, simama kwa miguu yako pamoja na hawa jamaa wawili vijana wanaosimama sasa. Inua . . . Mungu akubariki. Mungu awabariki kila mahali, hilo ni jema.

89 Mimi mwenyewe nimesimama, nataka Mungu anichunguze na kunijaribu, kama kuna kitu chochote kichafu ndani yangu, nifunulie, nitakiungama na kukisahihisha, nitaenda nifanye chochote anachotaka nifanye. Kwa maana kama nilikuwa nikifa, hicho kingekuwa ndicho kilio changu; kama ulikuwa unakufa, hicho kingekuwa kilio chako. Basi kwa nini usigeuke sasa kabla dhoruba haijaja, ili katika saa za shida yako uweze kusema pamoja na Ayubu: "Najua Mkombozi wangu yu hai"? Hivi hutasimama?

90 Kutakuwako na wengine zaidi kabla hatujaomba? "Nikumbuke, Ee Bwana." Mungu awabariki, akina mama. Mungu awabariki nyote. Endeleeni tu kusimama kwa ajili ya maombi. Naam, huko juu kwenye roshani, hilo ni jema. "Imani huja kwa kusikia."

91 "Nilizitafakari njia zangu, miguu yangu nikaielekeza kwenye shuhuda Zako, Ee Bwana." Huenda hatari ikawa mlangoni, ipo. Kama kuna chembe moja ya hukumu, simama kwa miguu yako sasa kwa ajili ya maombi.

92 Wakati wengi wamesimama, wengine wakisimama, Mungu awabariki, huo ni uaminifu. "Nilipozitafakari njia zangu, kwa kuwa nimetafakari yale nimekuwa, Bwana, ni—ninakugeukia Wewe." Siamini kuna mmoja wetu anayeishi kila siku, ila ambao inatubidi kumgeukia Yeye kila saa.

Ninakuhitaji Wewe, loo, ninakuhitaji Wewe;
Kila saa ninakuhitaji Wewe;
Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu,
Naja Kwako.

93 "Naja, Bwana, nimesimama, hivyo tu ndivyo ninavyoweza kufanya. Ninasimama kwa sababu nimeshawishika kwamba nimekosea, nami ni—ninaomba rehema Yako."

94 Sababu ya mimi kuendelea kushikilia, ni kwa sababu watu wanaendelea kusimama. Ninajuaje kwamba dakika moja tu zaidi huenda ikamaanisha tofauti ya mauti na Uzima? Katika saa moja ama mbili tangu sasa, mvulana fulani aliye na mvilio moyoni, mshtuko wa moyo, akijua ya kwamba anaenda kukutana na Mungu, na kitandani mwake, akipiga mayowe, aliwazia, "Vipi kama tu ningesimama pale usiku wa leo kanisani? Ninasumbuka sana sasa sijui la kufanya!" Simama sasa, rafiki yangu, njoo kwenye Chemchemi hii. Mungu atakupa rehema.

95 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuombe, kila mmoja kwa njia yako mwenyewe, ninyi mliosimama.

96 Bwana, kwa uchaji, na kwa utulivu, na kimyakimya, tunakuja Kwako kwa unyenyekevu, tukijua ya kwamba sisi si chochote chema kwa nafsi yetu. Hakuna uthabiti ndani yetu hata kidogo, tumechafuliwa kabisa, kwa kuwa tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja katika ulimwengu huu

tukisema uongo. Na asili yetu ni wenye dhambi, nasi tunahitaji neema Yako, Bwana, na rehema Yako, na utakatifu Wako, kwa kuwa hatuna kitu ndani yetu, na wala makanisa yetu au kanuni zetu za imani haziwezi kutuficha kamwe, ni majani ya mtini tu yaliyokataliwa hapo mwanzo na vivyo hivyo yatakataliwa kwenye mwisho.

97 Lakini tunaielekeza miguu yetu kwenye shuhuda Zako, kwenye Neno Lako, nasi tunakiri makosa yetu na dhambi zetu na kuomba msamaha Wako. Chochote unajisi wetu ulicho, Bwana, jalia Chemchemi pale ambayo yule mwizi alifurahia kuiona, na ioshe dhambi zetu zote. Tujalie, Bwana. Jalia tuondoke kwenye jengo hili usiku wa leo kama watoto wachanga waliozaliwa upya, wapya na safi. Na kama ungetuita kutoka katika dunia hii usiku wa leo, tunajisikia tungekuwa tayari kuondoka, kwa sababu miguu yetu imeelekezwa kwenye shuhuda Zako. Tulikuwa tumepotea kama vile nilivyokuwa mwituni, Bwana, na jinsi moyo wangu ulivyofurahi kuona ule mnara siku hiyo! Nayo mioyo yetu inafurahi usiku wa leo kuuona ule mnara wa Kalvari, ambapo tunajua ya kwamba kuna usalama, na—na hapo ndipo waliopotea huingia na kupatikana na kuelekezwa nyumbani.

98 Wabariki hawa wapendwa, wanaume hawa, wanawake hawa, wavulana, na wasichana wanaosimama, wakikiri makosa yao. Imeandikwa katika Neno, "Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe." Nao wamekuwa wakiwawazia. Na kama Daudi alivyokuwa, wanaweza kuwa na hatia ya mambo mengine kama Daudi alivyokuwa na hatia ya kumchukua mke wa Uria, bali Wewe ulisikia hilo, ulisikia maombi ya Daudi, Nawe, ingawa ulimfanya avune kile alichopanda, lakini alikuwa angali ni mtumishi Wako, ulimsamehe kwa sababu alikugeukia Wewe.

99 Kamwe hawakuliacha Kanisa usiku wa leo kama Yuda, bali wamekuja msalabani, hawatajaribu kunywa waisahau hii, wata—wataomba iondoke, watafanya kama Yakobo, watalia mpaka Malaika wa Mungu awabariki na kuondoa dhambi yote na aibu. Nami ninaamini utafanya hivyo sasa hivi, Bwana, kwa kuwa Wewe uliahidi jambo hilo. Tunaliamini katika Jina la Bwana Yesu.

100 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, nitawaulizeni ninyi ambao mmesimama kwa miguu yenu, mliosimama, mnaojisikia kwamba miguu yenu mumeielekeza kwa Mungu usiku wa leo, mwinulieni mikono yenu, na kama mimi . . . mkimwashiria Yeye, "Bwana, nimekuelekezea miguu yangu." Mungu awabariki. Asilimia mia moja mlielekeza miguu yenu kwenye shuhuda za Mungu. Atalitimiza. Yeye ataondoa kila dhambi, akupe amani na utoshelevu, mambo ambayo ulimwengu hauwezi kufanya.

101 Sasa kusanyiko linaweza kuinua vichwa vyao na kuwaangalia jamaa na wanawake wanaosimama karibu nanyi. Ninawatakeni, wanapoketi chini, muwape mikono, "Mungu

akubariki," na kuwakaribisha katika ushirika wa Yesu Kristo. Wale waliokuwa wamesimama, wakati wakiketi chini, hebu Wakristo walio karibu waseme, "Mungu akubariki, ndugu, na dada." Kama kulikuwa na jambo lolote baya, nawe ujisikie sasa ya kwamba yote yamekwisha, Mungu na akurehemu. Amina.

102 Kuna yeyote aliye mgonjwa miongoni mwenu? Inua mkono wako. Sasa wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, mlio na maradhi. Kama nilivyosema jana usiku, nimekuwa nje nikiomba, na—nataka jambo hili moja maishani mwangu: kwamba wakati ni—ninapoomba na—nataka kuamini ya kwamba nitapata kile ninachoomba.

103 Maskini ndugu mzuri, ambaye ni wa Assemblies of God, Louisville, Kentucky, Ndugu Rodgers, ninyi watu wa Assembly of God, mnamwona kwenye ninii chako—kitabu chako cha—cha mhudumu wenu, vyovyote mnavyokiita, yeye ni jamaa mzuri, mdogo. Alikuwa kwenye chumba changu cha kusomea yapata siku tatu zilizopita, nasi tulikuwa tukiomba, naye akasema, "Ndugu Branham, unafikiri tutakuwa na uamsho huko Louisville?"

104 Nikasema, "Natumaini hivyo." Naye akageuka kuniangalia. Nikasema, "Ndugu Rodgers, nilikutana na Mungu hivi majuzi kwenye lile pango. Siwezi kusema kwamba nafikiri hivyo, kwa sababu siwazii hivyo, lakini kuna jambo moja ninaloweza kuwa mwaminifu kulihusu: natumaini hivyo." Ninaamini, natumaini tutakuwa nao, lakini kusema ninawazia, siwezi kuliwazia, mimi—mimi siegemei upande wowote, Ni—ningetaka kuuona, bali sijui kama utakuwako au la.

105 Tunataka kuyachunguza maisha yetu na kuona kama kuna kitu chochote kichafu ndani yetu, na kama mioyo yetu haituhukumu, basi ombeni, unaweza kupokea kile unachoomba. Nitaomba kwa ajili ya uponyaji wenu, ninawatakeni mwombe kwa ajili ya uponyaji wenu, na kuombea uponyaji wa watu walioketi pamoja nanyi. Mungu atawaponya hao watu.

Na tuombe sasa.

106 Bwana, kama tu vile ulivyojeruhiwa kwa makosa yetu, katika shuhuda Zako imeandikwa: "Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Kuna wale ambao ni wagonjwa kimwili ambao hawawezi kukutumikia vizuri tu kwa sababu ni wagonjwa na wanajisikia vibaya. Wamehangaika na kuja kanisani, nao wameketi katika mkutano huu wakiwasikiliza wahudumu, watumishi Wako, wakizungumza, wako katika mateso na maumivu. Mungu, jalia kwamba hili litalitatua sasa hivi, kwamba mioyo yao itaugeukia ushuhuda Wako: "Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa Yako yote," na, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Na bila hukumu mioyoni mwetu, sasa tunakuamini Wewe, kwamba Wewe utatuponya na

kutuondolea magonjwa yetu yote. Tunaomba hili, katika Jina la Yesu, na ndivyo itakavyokuwa. Amina.

107 Kuna barua hapa, Bwana, na kadi ndogondogo na vifurushi vinavyowakilisha wagonjwa na wanaoteseka. Na tunafundishwa kwamba vilitoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo, vitambaa na leso, nasi tunajua sisi si Mtakatifu Paulo, lakini Wewe ungali ni Mungu. Na iwe hivyo, Bwana, ya kwamba wakati leso hizi zitakapowagusa wagonjwa, adui na awaachilie na wapate kuponywa, kwa kuwa tutafuatilia shuhuda za Mungu, shuhuda za Biblia Yake, nasi tunamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyetusafisha na udhalimu wote, na kutupa Roho Mtakatifu na uponyaji wa Kiungu sasa hivi. Katika Jina la Yesu Kristo.

59-0610 Nilipozitafakari Njia Zangu
Philadelphia Church
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org